

UFUNUO, MLANGO WA TANO

SEHEMU YA I



Asante sana, Ndugu Neville. Bwana akubariki, ndugu yangu.

² Habari za asubuhi, marafiki. Ni furaha asubuhi ya leo, majaliwa, ama majaliwa makuu, ninapaswa kusema, kurudi hapa maskanini tena na kuwa na wakati huu uliotengwa kwa ajili ya ibada yetu ya asubuhi na ushirika wa Neno la Bwana. Ninaamini ilisemwa wakati mmoja, “Nilifurahi walipotwambia, ‘Twendeni nyumbani mwa Bwana.’” Kuwa pamoja na Ndugu Neville tena, na marafiki zangu wazuri na wa thamani.

³ Pia nadhani ni baridi kidogo, ama joto kidogo kule nyuma. Nasi, nafikiri, tuna vipepeo ambavyo mnaweza kutumia kwa mikono yenu namna *hii*. Kama—kama . . . tunavyo vipepeo endapo mna mota, basi kuvifanya tu viendeele. Ama, tulikuwa na lundo lake hapa, nafikiri wangali wanavyo. Ninaona wengine wakitumia vitabu vya nyimbo ama kitu kingine. Na ni . . . jambo moja tunalojaribu kufanyia ibada, ni kukwepa sehemu hizi ambazo ziko—ziko katika siku za usoni zenye joto. Kwa hiyo sisi ni . . . Hiyo ndiyo sababu tupo hapa asubuhi ya leo, kuzikwepa sehemu hizo. Na jambo moja tu linaloweza kufanya hivyo, hiyo ni Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo inayofanya hivyo.

⁴ Nami nilifurahia sana kusikia taarifa nzuri ya kanisa, jinsi linavyoendelea, linavyoendelea na Bwana, na jinsi Mungu anavyowashughulikia katika karama za kiroho. Nami bila shaka ninamshukuru sana Mungu kwa ajili ya mioyo yenu miaminifu ambayo Yeye anaweza kuishughulikia, na kutumaini ya kwamba Yeye atawaweka papo hapo katikati ya ile Njia nyofu na nyembamba, kwamba hamtaenda kulia wala kushoto kutoka Kwake.

⁵ Nami ninataka kumshukuru Ndugu Colvin na binti yake, naamini ndio, waliokuwa hapa dakika chache zilizopita ambao waliimba wimbo ule, *Hakuna Machozi Mbinguni*. Huo ni mzuri. Bila shaka ninauthamini huo.

⁶ Na kama vile Ndugu Neville alivyosema kuhusu mimi na yeye miaka kadhaa iliyopita, nami ninaweza kusema hilo kumhusu Ndugu Colvin, tumefahamiana kwa miaka kadhaa. Na kumsikia akiimba nyimbo hizo za kale za Injili na kuwalea watoto wake katika njia ya Bwana, inausisimua sana moyo wangu. Inanifurahisha kujua ya kwamba Mungu angali ana watu wanaompenda na kumjali Yeye. Nasi tunashukuru kwa ajili ya hilo.

⁷ Sasa, tangu niliporudi, ninasikia kwamba wengi wamebatizwa katika Imani, nasi tuna furaha sana kwa ajili ya hilo. Ninamwona rafiki yangu mwema, Ndugu Elmer Gabehart huko nyuma. Ninasikia ya kwamba ndio kwanza abatizwe katika Imani, na bila shaka ninashukuru kwa hilo. Hiyo inalifanya kundi letu lote la kale la wawindaji huko chini Kentucky karibu tayari, kuchukua tu idadi iliyoruhusiwa pekee sasa, sivyo?

⁸ Ninakumbuka (Nami najua Rodney ananisikiliza kwenye chumba cha nyuma, iwapo yuko mle bado, naye Charlie ameketi mbele zangu.) tulipokuwa tukienda kule chini. Hao vijana wote walipenda kuenda, “Vema, ni kuchakulo,” wangewachukua wachache wa ziada kama wangewapata. Nami nikaanza kuwazungumzia na hilo halikuwa sahihi. Kwa hiyo sasa wao . . . kundi hilo lote karibu limeongoka nadhani itatubidi tu kuhamia huo mkoa mwingine na kuwanyosha huko. Hilo litakuwa sawa.

⁹ Kwa hiyo wakati mwingine mimi huangalia chini, kama vile kila mhudumu, chini kwenye njia ambayo umepitia, na kushangaa kuhusu ha—hayo mambo, kwamba kama—kama umepanda Mbegu.

¹⁰ Ninyi . . . wengi wenu mnamfahamu Johnny Appleseed katika . . . wa Marekani. Mbona, kulikuwako pia na m—mtu huko Uswidi ambaye alihesabiwa kitu kama hicho, yeye alipanda maua. Nao wanasema hiyo ndiyo sababu wanayo maua mengi sana ya kupendeza huko Uswidi sasa, na kwa sababu walipanda hizo mbegu za maua, popote angaliweza kupata kipande cha ardhi ambapo mbegu zingekulia. Yeye alipenda maua kwa hiyo alipanda tu mbegu kote. Yeye ameaga dunia lakini maua yake yangali yanaishi.

Na kuachana huacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;

Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
Wakati akisafiri bahari adhimu ya maisha,
Ndugu mpweke ambaye chombo
kimemwendea mrama,
Akiona, atatiwa moyo tena.

¹¹ Na hilo ndilo sisi sote tunataka kuona, jambo fulani ambalo tumefanya ambalo litawafanya wengine ku—kufaidika na yale tuliyoifanya.

¹² Siku chache zilizopita nilikuwa nimeketi, nikizungumza na maskini rafiki yangu mwaminifu hapa mjini, daktari wa tiba, Sam Adair. Naye akasema, “Unaendeleaje, Bill?”

¹³ Nami nikasema, “Loo, vizuri kabisa, nadhani, Dak.” Nikasema; “Nawe je?”

¹⁴ Naye akasema, “Loo, wagonjwa wengi sana.” Kasema, “Nilikuwa na uchunguzi kumi na tano alasiri ya leo.”

15 Nikasema, “Vema, hilo ni sawa mradi tu ni kufanya uchunguzi tu pasipo kupata tatizo lolote.” Nikasema, “Unajua, ninii...” Tukaanza kuzungumza kuhusu huko nyuma wakati tulipokuwa vijana. Nami nikasema, “Vema, Dak, sijui kabisa nitakuwa huku muda gani. Sote wawili tuko kwenye umri wetu wa miaka hamsini na kitu.”

Naye akasema, “Hiyo ni kweli, Bill.”

16 Nami nikasema, “Lakini miaka hii yote, yapata miaka thelathini na moja ya huduma sasa, nimeuweka moyo wangu tayari kwa ajili ya saa hiyo hapo Yeye atakapokuja. Kwa hiyo haijalishi ni lini Yeye atakapokuja.”

Kwa hiyo akasema, “Hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Msisimko mkubwa kuliko wote nilio nao ni kuishi kwa ajili ya wengine.”

17 Naye akasema, “Hivyo ndivyo maisha yalivyo, inafanya maisha kuwa halisi, ni wakati wewe...si yale unayoweza kufanya ama kufanikisha kwa ajili ya nafsi yako, bali ni yale unayoweza kufanya kwa ajili ya wengine.”

18 Mnaona, hapo ndipo kweli unaishi. Na kukitokea kuwapo na mtu mmoja miongoni mwetu ambaye hajawahi kufanya hivyo, kujaribu kuishi kwa ajili ya mtu mwingine, hebu jaribu hilo, na uone tu jinsi maisha yalivyo na mengi kwa ajili yako wakati hutaishi kwa ajili ya yale unayoweza kupata mwenyewe kutoka katika maisha bali yale unayoweza kumpa mtu mwingine maishani. Nawe utaona kwamba imebarikiwa zaidi kuliko utajiri ama chochote cha...ambacho kinaweza kuwaziwa. Ni yale unayoweza kumfanyia mtu mwingine kuifanya mizigo ya maisha...Ambapo, maisha yenyewe ni mzigo. Nalo litaufanya mwepesi kidogo kwa ajili ya mtu mwingine. Huijui tu ile furaha isipokuwa uwe umejaribu wakati mmoja, kufanya jambo fulani kwa ajili ya mtu mwingine.

19 Ndipo basi hilo linanileta kuwazia juu ya miaka thelathini na moja (itakuwa hivi karibuni) ya huduma ya Bwana. Nami nakisia kila mtu huwazia juu ya wakati fulani ambapo hana budi kuja kwenye huduma yake ya mwisho na kuifikia saa yake ya mwisho, na kuangalia nyuma njiani na kuona yale yaliyotimizwa, kuona yale yaliyotendeka, “Umefanya chochote?” Na endapo...Ndio kwanza niseme, yale unayowafanyia wengine ndiyo muhimu.

20 Mara nyingi ninashangaa itakuwaje nitakapofikia mwisho wa safari yangu, ambayo hatujui hiyo itakuwa ni wakati gani, hakuna hata mmoja wetu. Kwa hiyo nilikuwa nikiwazia kuhusu kuangalia nyuma kwenye mburuzo ambako nimepitia maishani na kuona vilima mbalimbali na sehemu za michongoma na mawe na mahali pagumu na mapito rahisi, na kile nilichofanya katika nyakati kama hizo. Yote yatajitokeza moja ya siku hizi kwenye ile saa ya kuondoka kwangu. Nayo itafanya hivyo kwa kila mmoja

wetu. Sote tutakuwa na hakika ya jambo hilo, ya kwamba ita— itajitokeza kwa kila mmoja hapo wakati huo utakapokuja.

²¹ Basi hilo linanileta ama linanipelekea kusema jambo fulani ambalo afadhali nikimbie kuliko kulisema. Linanipelekea kusema jambo fulani ambalo mimi... Huumiza moyo wangu kabisa kulisema, bali lile ninalosema ninalazimika kulisema, nikitambua kwamba hili linarekodiwa nao ulimwengu utalisikia, bali nimeondoka hudumani kwa ajili ya sa—sababu ambayo ninasikitika kwamba sina budi kuondoka kwa ajili yake. Na labda wengi wenu mmelisikia, mimi kuifunga ofisi yangu, na kadhalika, na kuondoka hudumani.

²² Sijui ambako Bwana wetu ataniongoza, wala hilo siwezi kulizua, ama chochote Yeye atakachoniongoza kufanya. Lakini ninawazia mwishoni mwa safari ambapo sina budi kuja. Na chini kwenye safari ya maisha nimefanya makosa mengi ambayo ninayasikitika sana kutoka moyoni mwangu, kwa sababu, nadhani, kuwa mwanadamu na katika udhaifu na kadhalika, humfanya mtu kufanya mambo ama kusema mambo ambayo... na hata kutenda ambavyo wasingetaka kutenda vinginevyo. Lakini kwa kuwa ni udhaifu wa binadamu, mbona, tu—tunazo nyakati hizo. Lakini kuna...

²³ Kama kuna jambo lolote ambalo limekuwa moyoni mwangu kufanya, lilikuwa ni kuyasikia Maneno hayo ya Bwana wetu Yesu mwishoni mwa safari hii, kusema, “Ilifanywa vema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu.” Na mara nyingi nimesema ningetaka kuwa nimesimama pale wakati Yeye aliposema, “Njoni Kwangu”; bali kweli nilitamani kusikia ikisemwa, “Umefanya vema.” Kwamba sikuisikia ile Sauti, katika asili, ikisema, “Njoni Kwangu,” huko nyuma katika zile nyakati za kule kuandikwa kwa Biblia; bali ninatamani kuisikia ikisema, “Umefanya vema.”

²⁴ Na kama kuna chochote nilichotaka kuwa, na shauku za moyo wangu kuwa, ilikuwa ni mtumishi wa kweli wa Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wangu. Ninataka ushuhuda wangu uwe safi, dhahiri, kwamba nilisimama, katika makosa yangu yote ningali nilimpenda Yeye kwa moyo wangu wote. Nami nafanya hilo asubuhi ya leo kwa moyo wangu wote.

²⁵ Na, kwa sababu ya jambo hilo, inanilazimu kusema ninaiacha huduma, ni kwa sababu kuna jambo fulani lililoibuka miongoni mwa watu lililonifanya kufanya hivyo, hilo ni, kwamba nimeondolewa kwenye kitengo changu cha “mhudumu” ama “ndugu” na kuitwa Yesu Kristo, na kuitwa hivyo...basi hilo lingenifanya kuitwa mpinga Kristo. Nami nitakutana na Mungu kama mwacha kazi kabla sijakutana na Yeye kama mpinga Kristo kuondoa kutoka Kwake.

²⁶ Nilisikia juu yake miaka mi—michache iliyopita nami nikafikiri ilikuwa ni mzaha. Ndipo nikakutana na ndugu kadhaa

(ambao sioni yeyote wao mkutanoni asubuhi ya leo), wawili ama watatu wao wakati mmoja kwenye ziara ya kuvua samaki, nao wakanijia kwa hoja ya kusema, “Ndugu Branham, hivi wewe si Masihi aliyetiwa mafuta, yule Kristo?”

²⁷ Ndipo nikaweka mikono yangu shingoni mwa hao ndugu wawili, ama, wote, nami nikasema, “Ndugu zangu, kadiri ambavyo nimejaribu kuwa mtumishi wa kweli wa Kristo, nisingewataka ninyi kusema jambo kama hilo. Na endapo kamwe lingesemwa juu yangu, basi nitaondoka hudumani nikiwa na dhamiri safi, nanyi mnaofanya jambo hilo mtawajibika kwa kila nafsi ambayo ningeiokoa kwenye wakati huo; mnaona, kwa kuniondoa hudumani.” Nami nilifikiri hilo lililimaliza.

²⁸ Kisha nikalisikia mara zingine chache. Lakini haikuwa hivyo. Ndipo hivi majuzi huko Canada ndugu mmoja alinionyesha kitu kama kijikaratasi kidogo alichokuwa amebeba mfukoni mwake, kilichosema, “William Branham ni Bwana wetu,” wakibatiza katika jina la William Branham. Ndipo maskini...wa thamani...Kama ingalikuwa ni adui, kama ingalikuwa ni adui wangu ningalijua ilikuwa ni mzaha. Lakini ndugu wa thamani, mpendwa alikuja kuungama dhambi zake na makosa yake na kusema imani yake kwangu mimi kuwa ni Yesu Kristo.

²⁹ Nami ninazo barua nyumbani, na simu kutoka Chicago na mahali mbalimbali, zikiniuliza kama ninaamini fundisho hilo la sharti.

³⁰ Nami nina kila namna ya barua ambazo zimekuja katika siku chache zilizopita, na simu kutoka sehemu mbalimbali, kwa hiyo, wakisema kwamba nilikuwa Kristo. Ndugu zangu, huo ni uongo mwovu wa kuchukiza sana, wa aibu, ulio wa ibilisi! Mnaona? Mnaona, mimi ni ndugu yenu. Sasa, hilo lingemwondosha mtu yeyote hudumani. Hilo lingemfanya mtu yeyote anayempenda Kristo kukitoroka kitu hicho hicho.

³¹ Nilimwendea Bwana hapa si muda mrefu uliopita, nilipolisikia kwa mara ya kwanza, yapata mwaka mmoja uliopita. Kisha nikamwendea Bwana Naye akanirejesha kwa Maandiko ambapo Yohana alijitokeza akihubiri, kwamba hawakuwa na nabii duniani kwa miaka mingi sana, mpaka ingekuwa...wote walishangaa mioyoni mwao, wakifikiri labda Yohana alikuwa ndiye Masihi. Kwa hiyo basi mimi...Yohana, walienda na kumwuliza, naye akasema kwamba hakuwa. Mlisoma hilo katika Luka mlango wa 3, kifungu cha 15. Na kwa hiyo basi...Lakini hayo kidogo yalitulia, kwa hiyo nikayaacha yaende namna hiyo.

³² Lakini basi ilipofikia kwenye jambo hili, basi nilijua jambo fulani halina budi kufanywa. Basi nasema hivi, “Ya kwamba yale maono na yule Malaika wa Bwana aliyeonekana huko mtoni,”

(endapo huu utakuwa ndio ujumbe wangu wa mwisho ama jambo la mwisho kwa kanisa, kwa ulimwengu) “mambo hayo ni ya Kweli, kuhusu yule Malaika wa Bwana.”

³³ Nami nilitulia kama watu waliniita nabii mara nyingi, maana *nabii* katika agano la Kiingereza ni “mhubiri, mtabiri, mbashiri wa Neno” tu, na kadhalika. Ningeumilia hilo maana kwa namna fulani ungeweza tu kulisukumia hilo chini; bali inapofikia kuitwa “Kristo aliyetiwa Mafuta,” ama kitu fulani, hilo lilingizidia mno. Kwa hiyo nisingeweza kabisa kuvumilia hilo.

³⁴ Na kwa hiyo basi yapata . . . Nilikuja . . . Baada ya kuondoka mkutanoni huko Canada, nilikuta kwamba huko juu sana kwa Waeskimo ama Wahindi huko juu, lilikuwa limeingia miongoni mwao.

³⁵ Na kwa hiyo likanihuzunisha kabisa. Nayo ziara ya mawindoni niliyokuwa nimepanga kwa muda mrefu, nisingeweza kuifanya. Nilihofia ajali ya mawindoni, kama mnafahamu ninayomaanisha. Nilitetemeka sana, vibaya kuliko ninavyosimama hapa sasa. Wala kamwe nisingeweza kulivumilia zaidi, kuwazia ya kwamba miaka thelathini na mmoja ya huduma iliteremka kwenye mfereji wa maji machafu ya ibilisi, ikaingia katika . . . Nitakapokuwa nimeondoka, wao watasema nini? “Huyo hapo, hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa”; na ushawishi wote niliokuwa nao juu ya watu, basi mnaona mahali lingekuwa, ningekuwa mpinga Kristo. Nami kamwe nisingeweza kulivumilia!

³⁶ Nikawaza, “Afadhali nife hapa misituni, kana kwamba niliangukia bunduki yangu ama kitu fulani, kuliko . . .” Nami niliona nilikuwa . . . Ndipo nikawazia juu ya maskini mtoto wangu Joseph, na kadhalika, ambaye alipaswa kulelewa. Wala sikuwa katika hali ya kuwinda, kwa hiyo niliondoka tu mwituni nikaja nyumbani.

³⁷ Nami nimekuwa nimehuzunika sana yapata siku nane ama kumi, nikiwa kwenye matatizo makubwa sana hata ni—nilifikiri nilikuwa ninaingia kichaa. Ndipo nikamwomba tu kila mtu asinikaribie na waniache peke yangu maana niko na matatizo na wasiwasi mkubwa sana na fadhaa na kuvurugika kabisa.

³⁸ Ndipo nikashangaa; kama ingalikuwa ni adui fulani wangu, ingekuwa ni sawa, bali ningalilicheka tu na kusonga mbele; bali inapofikia kuwa ni ndugu wa thamani, dada wa thamani, basi hilo ndilo linaloniumiza mimi. Kisha nikasema, “Bwana, ninii kuu . . . jambo hili limenizidia sana, itanibidi tu kuondoka na kuliacha mikononi Mwako. Si—sijui lingine lolote la kufanya.”

³⁹ Siku chache zilizopita usiku, kulihakikisha, Bwana ali—alinizuru. Ndipo nikamwona wa thamani . . . mtoto . . . nyo—nyoka ambaye alikuwa ni wa manjano na mweusi, na kuniambia moja kwa moja, basi ki—kitu hicho kikaniuma mguuni. Lakini

damu ilikuwa nzuri sana hata haikunidhuru. Nami nikaangalia chini, na hapo ndipo nilipokuwa nimeumwa hapo mbeleni. Ndipo nikageuka upesi pamoja na bunduki na kukipiga ki—kitu hicho, nayo ikakipiga papo hapo katikati ya kitu hicho.

⁴⁰ Ndipo ndugu fulani akasema . . . niligeuka na bunduki yangu kumpiga risasi kichwani, naye akasema, “Usifanye hivyo, okota tu kijiti hicho kilicho hapo karibu nawe.” Ndipo nilipougeuza mgongo wangu kukiokota hicho kijiti, alijifurukuta akaingia majini, kidimbwi kidogo tu cha maji.

⁴¹ Nikasema, “Vema, hawezi kudhuru kwa muda mwingi zaidi sasa kwa kuwa ninaamini ndugu anatambua (hao ndugu) yale yangetukia.” Nikasema, “Ataninii . . . Amejeruhiwa vibaya sana, kwa hiyo atakufa.”

⁴² Nami ninawauliza wengi wa washiriki wa kanisa langu hapa, katika maskani hii pamoja na mimi na Ndugu Neville, ambao wamenijia na swali lilo hilo: Ndugu, dada, hivi sijajaribu kuwa mtumishi wa kweli wa Kristo mbele zenu? Hivi sijajaribu kuwa ndugu yenu? Sasa, popote pale, ni roho juu ya watu wa thamani. Watu wengi wameniliza hilo. Lakini ni—ni roho fulani, bali natumaini ya kwamba leo hii itapokea jeraha la kufisha nayo itakufa upesi kusudi niweze kurudi hudumani. Mpaka wakati huo, nitawaomba kila mmoja wenu, mniombee. Sijui nitakalofanya. Mahali pangu panauzwa. Siwezi kabisa kulivumilia, ni—ni—nikikaa huku, nitaingia wazimu kabisa. Nami . . . ninawaulizeni mniombee.

⁴³ Basi, kumbukeni, kama mmewahi kuniamini, kama mmewahi kuniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Kristo, kumbukeni, “Hilo ni kosa! Ni makosa!” BWANA ASEMA HIVI! “Ni makosa! Msiwe na uhusiano wowote nalo!” Mimi ni ndugu yenu.

Na tuinamishe vichwa vyetu:

⁴⁴ Baba wa Mbinguni, mwili wangu unatetemeka, mikono yangu inajikunyata pamoja, vidole vyangu vimekunjamana ndani ya viatu vyangu. Ee Mungu, nirehemu. Kwani nimewahi kufanya nini, Bwana, kustahili haya? Ninaomba kwamba utanirehemu sana, Bwana, na wote. Na huko juu, na hao watu wapendwa wa thamani, jalia waone kosa lao na yale wametenda, Bwana, kuuvunja moyo wa ndugu yao na kuninii . . . sio tu ndugu, bali Mwokozi wetu, Baba yetu wa Mbinguni. Ninaomba ya kwamba utatusamehe makosa yetu, Bwana. Jalia Damu takatifu ya Kristo sasa iuvute utu wetu pamoja, Bwana, na kibarikiwe Kifungo kiifungayo mioyo yetu katika upendo wa Kikristo na ushirika.

⁴⁵ Mungu, jalia adui aliyewaendea ndugu zetu na dada zetu pamoja na . . . jalia apokee jeraha la kufisha asiweze kuishi tena; jalia afe tu kabisa, Bwana. Ukifanya hivyo, Baba, nitarudi hudumani tena. Lakini mpaka wakati huo, Bwana, mimi ni

mtumishi wako aliyevunjika moyo, nikingojea, nikingojea. Ni zaidi ya chochote niwezacho kufanya. Kwa machozi na pamoja na kilio na kushawishi nilijaribu, Bwana, sana (Unaujua moyo wangu.) kulikomesha kabla halijafika umbali huo, bali lilienda kupita chochote ningaliweza kufanya. Kwa hiyo, Baba, ninalikabidhi Mikononi Mwako kutoka kwenye mimbara hii kufikia mahali ambapo nimehubiri kwa miaka hii yote. Ninalikabidhi Mkononi Mwako.

⁴⁶ Sasa, Wewe ulishughulikie, Baba, katika njia Yako Mwenyewe ya Kiungu. Na hapo litakapomalizika kabisa na kila kitu kimekwisha, basi mtumishi Wako atarudi. Mpaka wakati huo nitakuwa nikingojea kusikia kutoka Kwako, Bwana.

⁴⁷ Tubariki sasa na utupe ibada kuu leo; kwa kuwa tupo hapa sio hasa kwa ajili ya hili, bali kulifanya tu dhahiri, hadharani, mbele ya walimwengu. Wapate kujua, Baba, ya kwamba ninakupenda na ninakuamini Wewe na nimekutetea, na—na ninataka kufanya hivyo. Ikinibidi kuondoka, jalia niondoke, Bwana, kwa moyo safi na kumbukumbu halisi ya kwamba nilikuamini na kukutumaini Wewe. Tujalie. Nami nitakusifu nasi kukupa Wewe utukufu katika nyakati zote zijazo kupitia Yesu Kristo. Amina.

⁴⁸ Sasa, kwenye Maandiko, hebu tuifungue Biblia kwenye... Niliwazia asubuhi ya leo lingekuwa ni jambo zuri, endapo Ndugu Neville hajali, kuendelea tu kwa dakika chache katika...

⁴⁹ Sasa, mimi... Hebu nisilisikie mara nyingine moja likitajwa miongoni mweni. Ombeni tu na kuliweka nje, mkalifungie nje. Mnaona? Sininii... Ni—nina—nina umri wa miaka hamsini na miwili, bali nafikiri labda, kama Mungu akiniachilia, nina maisha kidogo yaliyosalia, na ninataka kutumia kila wakia wa wakati wangu kwa ajili ya Kristo. Kwa hiyo, kumbukeni, ninaondoka kwa sababu nimesukumwa kufanya hivyo.

⁵⁰ Sasa, katika Kitabu cha Ufunuo, katika mlango wa 4 ambapo tuliachia hivi majuzi tulipokuwa tukisoma... Ufunuo, mlango wa 4, ninaamini, kwenye sehemu ya mwisho ya kile kifungu, ya huo mlango. Vema, ni wangapi wanaopenda Ufunuo? Ajabu! Sasa, ninaamini tuliachia kwenye mlango wa 5—wa 5, sivyo? Tuliachia, kwenye mlango wa 4, wale Wenye Uhai wanne. Sasa, hebu tuliendee Neno sasa, tukiyasahau mambo hayo yaliyo huko nyuma.

⁵¹ Baba Mungu, tusaidie sasa kwa kuwa tuna wasiwasi, bali tunalikaribia Neno. Tukiyasahau yale yaliyo nyuma, tunakaza mwendo sasa tuifikilie mede ya wito mkuu, wito mkuu wa huduma ya kuwa mtumishi wa Kristo. Utupe Neno asubuhi ya leo na uzilishe nafsi zetu zilizo na njaa, kwa kuwa tuna shauku, Bwana, na kuungojea ule upako wa thamani wa Roho Mtakatifu. Njoo miongoni mwetu, Bwana, ukitusamehe dhambi

zetu na makosa na kutuacha tuwe watumishi Wako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁵² Sasa, tulizichukua nyakati za kanisa, zile Nyakati Saba za mwisho za Kanisa. Halafu basi, sasa, ninaamini baadhi yao wanajaribu kuninii. . . wataziandika hizi, nyakati za kanisa. Ndipo tunaingia katika mlango wa 4 wa Kitabu cha *Ufunuo Wa...* Ni kitu gani hiki? *Ufunuo Wa Yesu Kristo. Ufunuo*, unaoitwa katika Kilatini, *Apokalipsi*, ambalo linamaanisha “kufunuliwa, ku—kuondoa kifuniko, kuonyesha, kuweka wazi,” kuuelezea ufunuo wa Yesu Kristo ambaye Alikuwa, Aliyeko, na Atakayekuja, Shina na Mzao wa Daudi.

⁵³ Sasa, katika mlango wa 4, tunaona ya kwamba Yohana alinyakuliwa Mbinguni baada ya kuziona zile nyakati za kanisa. Kuweka tu msingi kidogo sasa, na halafu tutaninii. . .

⁵⁴ Labda ni bora zaidi kusoma vifungu vichache vya mlango wa 5, na kisha tutaanza moja kwa moja kwenye msingi.

Kisha nikaona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi kitabu kilichoandikwa ndani na. . . nyuma, kimetiwa muhuri saba.

Nikaona malaika mwenye nguvu akitangaza kwa sauti kuu, N'nani astahiliye kukifungua kitabu, na kuzivunja muhuri zake?

Wala hapakuwa na mtu mbinguni, wala juu ya nchi, wala chini ya nchi, aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama.

Nami nikalia. . . kwa kuwa hapakupatikana mtu astahiliye kukifungua na. . . kukisoma hicho kitabu, wala kukitazama.

Na mmojawapo wa wale wazee akaniambia, Usilie: tazama, Simba wa kabila la ninii. . . la Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na zile mihuri zake saba.

Nikaona, na, tazama, katikati ya kile kiti cha enzi. . . wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote.

Akaja, akakitwaa kile kitabu katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi.

Hivyo ni vifungu vya kwanza saba.

⁵⁵ Sasa, sasa, katika mlango wa 3 wa Ufunuo, tunaona mwisho wa Wakati wa Kanisa, ambao uliishia na Laodikia, ule wakati vuguvugu wa kanisa. Basi tunaona ya kwamba, mara baadaye, Yohana alitwaliwa katika Roho, juu Mbinguni. Naye akaona

mambo yaliyokuwako, na yatakayokuja, na mambo yaliyokuwa yamekuwako. Sasa, tunaona ya kwamba, kanisa halionekani tena mpaka kwenye mlango wa 19 wa Ufunuo, ndipo linarudi pamoja na Bwana wake, limeoshwa vizuri sana katika Damu.

⁵⁶ Sasa, katika nukuu hili la mwisho, kwa ajili ya msingi mdogo kuketi mahali Yohana alipo sasa, tuliona ya kwamba katika ule ujumbe wa mwisho... nilikuwa tu nikiuangalia kwa kifupi jana, baadhi ya muktadha niliokuwa nimezungumzia. Naye Yohana alichukuliwa juu Mbinguni na kuyaona hayo mambo. Nami nilikuwa nimeona mle ndani ya kwamba Yeye alikuwa amenipa ufunuo, kwamba... Mwajua, baada ya kufufuka Kwake wengi walikuwa pamoja Naye, ndipo baadhi yao wakasema, “Itakuwaje kwa mtu huyu anayeegemea kifuani Mwako (Yohana)?”

⁵⁷ Yesu akageuka na kusema, “Imewapasaje kama akikaa hata nijapo?” Kwa hiyo Yeye kamwe...

⁵⁸ Ndipo likatokea fundisho. Mnaona jinsi linavyoweza kuanza kwa urahisi? Likatokea fundisho kwamba—kwamba “Yohana hataona mauti mpaka atakapomwona Yesu akija, ama mpaka kule Kuja kwa Pili.” Biblia ilisema lilienea fundisho fulani lililotokana na hilo.

⁵⁹ Walakini, Yesu kamwe hakulisema namna hiyo. Yeye alisema, “Inawapasaje ikiwa atakaa hata nijapo?”

⁶⁰ Sasa, tunaona ya kwamba yeye aliinuliwa juu mbinguni na kuona tangu wakati huo hata kule kuja kwa Bwana, kana kwamba alikuwa kule na kuliona lote likitukia. Yohana mwenyewe hakuishi... Aliishi akawa mwenye umri wa miaka tisini na kitu, kisha akafa kifo cha ka—kawaida (yule wa pekee wa wale mitume) akiisha kutoka kwenye uhamisho wake kutoka kisiwa cha Patimo.

⁶¹ Sasa, kuna jambo moja muhimu sana ningetaka... (nafikiri wameuchukua ninii wangu... wameuondoa ule ubao, lakini...) Ningetaka kulitilia mkazo kidogo kabla hatujalifikia jambo hili muhimu sana. Loo, huu ni adhimu! Mlango wa ajabu, wa ajabu sana.

⁶² Na halafu mlango huo mwingine unaanza na kule kufunguliwa kwa mihuri hii. Loo, jamani! Na halafu inatupasa kuruka kutoka hapo na kwenda mahali mbalimbali katika Biblia, kuipata mihuri hii hapo itakapofunguliwa na jinsi siri zao zilivyo. Loo, ni adhimu sana, zimejaa kabisa vitamini za kiroho!

⁶³ Sasa, tunaona kwamba moja ya mambo makuu yaliyo mazuri sana ningetaka kuvutia usikivu wenu kwake, yalikuwa ni wale Wenye Uhai (wa sehemu ya mwisho ya mlango wa 4) ambao Yohana aliwaona wakiliangalia lile Sanduku la Agano. Mnakumbuka jinsi walivyowekwa kama tu Israeli katika safari yake? Walikuwa, sasa, hapo juu, kulikuwako na uso wa Kiumbe

hai. Nasi tuliona ya kwamba Viumbe hawa hawakuwa ni Malaika, wala hawakuwa ni wanadamu. Walikuwa ni Makerubi. Nasi tuliwaona katika Agano la Kale pamoja na lile sanduku. Tunawaona katika Agano Jipya. Kisha tunawaona huko katika kule Kuja kwa Bwana tena, Makerubi wakikilinda kile kiti cha rehema.

⁶⁴ Kiti cha rehema ambacho hakuna mtu angaliweza kukikaribia isipokuwa pawe na upatanisho pale kwa ajili ya mtu huyo, njia pekee ambayo madhabahu...Wakati yaliponyunyiziwa damu, basi yakawa ni kiti cha rehema. Bali baada ya hiyo damu kuondolewa, basi yakawa ni kiti cha hukumu.

⁶⁵ Na, loo, jamani, hakuna mtu angaliweza kuzistahimili hukumu za Mungu. Jambo pekee tunaloweza kutazamia ni rehema, sio hukumu, sio haki...haki. Hatuwezi kuikaribia haki Yake; kwa sababu, haki Yake, itambidi kulitimiza Neno Lake; na kulitimiza Neno Lake, "Siku utakapokula, siku hiyo utakufa." Ni nani angetaka haki? Sitaki haki. Ninaomba rehema. Jamani, jalia rehema ya Mungu...Nacho kiti cha rehema kimenyunyiziwa!

⁶⁶ Lakini kulikuwako na wakati wa kuyasafisha madhabahu, wakati yalipokuwa ni kiti cha hukumu mradi tu damu ilikuwa imeondolewa kwenye hicho kiti.

⁶⁷ Sasa, tunaukaribia wakati huo *sasa*. Sasa tunakaribia, katika wakati huu, kusafishwa kwa madhabahu na hukumu zinazokuja juu ya nchi. Mnaona? Mradi tu Damu imo mle, Mungu hawezi kuiangamiza dunia; mradi tu Damu ipo pale, hakuna aliye mwenye dhambi mbele za Mungu. Kila mtu yuko sawa, kwa sababu kuna Upatanisho kwa ajili ya kila mtu. Lakini ukikosa kuukubali Upatanisho huo na kwenda Mbele Zake, ndipo wewe ni mwenye dhambi, umepita hiyo rehema. Ndipo basi umejihukumu mwenyewe. Lakini sasa kukiwapo na rehema... Lakini hapo kusafishwa kwa madhabahu kunapokuja, Damu inaondolewa kwenye kiti cha rehema na halafu ghadhabu ya Mungu inaanguka juu ya nchi. Loo, jamani! Mungu aturehemu, kwamba tusikutwe katika siku hiyo bila rehema za Mungu.

⁶⁸ Sasa, tunaona mle ndani...Nitajaribu kwa namna fulani kulifanya la kiroho hapa, ama kulichora kwenu kwa mikono yangu, kwamba kulikuwa na pembe nne jinsi Israeli walivyopiga kambi wenyewe. Waliliweka sa—sanduku katikati, na kwenye pande nne za hema kulikuwako na makabila matatu ya Israeli, na tatu nne ni kumi na mbili, ama nne tatu, hasa, kumi na mbili. Na kila moja ya hizo tatu ilikuwa na kiongozi. Na kila kiongozi wa kabila...

⁶⁹ Mmoja wao alikuwa ni Rubeni, sikuzote alipiga kambi ku—kusini. Alikuwa ndiye kichwa cha mwanadamu. Naye Efraimu alikuwa magharibi, pamoja na makabila matatu, alikuwa ni—ni

maksai. Ninii . . . Halafu mashariki kulikuwa na Yuda, ambaye ni simba. Na kaskazini kulikuwa na Dani, ambaye alikuwa ni tai. Sasa, angalieni. Mnawakumbuka? Ninyi nyote mnawakumbuka hao vizuri, jinsi tulivyowachora: yule tai, na maksai, na—na mwanadamu, na simba.

⁷⁰ Sasa, mnaona, Yuda analinda lango la mashariki. Naye Kristo ndiye “Simba wa kabila la Yuda.” Yeye atashuka kutoka anga za mashariki, aingie kwa njia ya lile lango. Yeye anakuja kutoka kwenye lango la mashariki kutoka kwenye kabila la Yuda. Na Yeye ni “Simba wa kabila la Yuda.”

⁷¹ Nasi tunaona, kwenye ujumbe wetu ujao asubuhi ya leo, kwamba Yeye angali anatangazwa “Simba wa kabila la Yuda, Shina, ule mwanzo hasa wa Daudi.” Daudi alikuwa ni mfalme, Milele. Naye Kristo anaketi juu ya kiti cha enzi cha Daudi katika ule Utawala wa Miaka Elf, ambaye ni Mfalme wa Milele. “Hatakosekana mmoja wa Daudi.” Haleluya! “Kamwe hatakosekana mmoja wa Daudi!” Mungu aliahidi hilo, kasema, “Hakuna atakayekosekana wa Daudi, hata mmoja.”

⁷² Mnasema, “Vipi kuhusu siku hizi, wako wapi hao mahakimu wa Kiyahudi?”

⁷³ Yeye angali ana yule Mzao, Kristo ni Mwanawe kulingana na mwili. Hapo mmoja ameketi pale. “Daudi hatakosai.” Hiyo ni kweli. Naye Kristo ndiye yule “Simba wa kabila la Yuda” kutoka mahali Daudi alipochipukia.

⁷⁴ Sasa, tunaona ya kwamba walikuwa ndio walinzi wa kiti cha rehema. Walikiangalia kile kiti cha rehema. Hakuna kitu kilichokuja kwake, kilivuka hayo makabila kwanza kabla hakijaweza kukifikia kile kiti cha rehema. Kila mtu aliyekuwa tayari kutoa maisha yake, kila Mwisraeli kambini angekufa kabla kitu chochote kuingia kwenye kambi hiyo kule na kukitwaa hicho kiti cha rehema. Na sasa tunaona ya kwamba huo ulikuwa ndio utaratibu wa Agano la Kale.

⁷⁵ Na katika utaratibu wa Agano Jipya tunaona jambo lile lile, kwamba kililindwa, kile kiti cha rehema. Loo, natumaini mnalipata! Kiti cha rehema kingali kinalindwa, kingali kina walinzi. Tuliona ya kwamba walinzi hao walikuwa ni Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, wakikilinda Kitabu cha Matendo, matendo ya Roho Mtakatifu yaliyotendwa miongoni mwa mitume, ambacho ni Ki—Kitabu cha Matendo cha lile Jipya la Agano Jipya. Na wale waandishi wanne wa hizo Injili, Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, wote wanakilinda kiti cha rehema kuonyesha ya kwamba ni Mungu, Roho Mtakatifu leo hii. Kila Andiko, Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, kila moja la hayo litaunga mkono Injili ya kweli ya Bwana Yesu Kristo na Matendo ya Roho Mtakatifu.

⁷⁶ Sasa, tunapoenda zaidi ya Hilo basi hilo Silo. Lakini linaunga mkono Ujumbe wa kweli! Kama vile tunavyoona

katika Matendo 2:38, ambapo, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu.”

⁷⁷ Na siku hizi wamelichukua Jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” kubatizwa kwalo. Hakuna Andiko kwa hilo! Hakuna msingi. Hakuna—hakuna kitu cha kulinda hilo, hata kimoja! Mnasema, “Mathayo alilisema.” Mathayo alilinda Hilo. Mathayo 28...1:18 kasema:

...kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Wakati...Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

Haya yote yalifanywa wakati...Yusufu mumewe, (hasa) akiwa ni mtu wa haki,...asitake kumwaibisha, aliazimu ku—kumwacha kisiri, hivi.

Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo: kwa maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

⁷⁸ Basi, Roho Mtakatifu na Mungu Baba ni Mtu yule yule la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili. Mnaona? Kwa hiyo mnaona!

Naye atamzaa mwana,...utamwita jina lake YESU:...

...na hayo yamekuwa, ili litimie...lililonenwa na...nabii,...

⁷⁹ Mungu angekuwa pamoja nasi, anayelitwa Imanueli, ambaye ni Mungu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, katika Jina moja (Yesu Kristo) ambalo linalinda lango hilo dhidi ya makosa.

⁸⁰ Siku chache zilizopita huko Chicago, mbele ya shirika la wahudumu wa Chicago, Chicago ya juu...Nilijua...Roho Mtakatifu aliniamsha usiku na kuniambia, “Simama karibu na dirisha.” Kasema, “Kunalo kundi la wahudumu nao wanaandaa kiamshakinywa kwa ajili yako.” Kasema, “Kuwa mwangalifu, watakuhambulia juu ya jambo hili.”

⁸¹ Nikasema, “Asante, Bwana.” Akanionyesha mahali kitakapofanyiwa.

⁸² Nami nikaenda nikawaambia baadhi ya wahudumu, Ndugu Carlson na Ndugu Tommy Hicks, jinsi ingalikuwa. Nikasema, “Mahali pale mlipopaagiza, haitakuwa hivyo. Tutakuwa mahali pengine.” Nikamwambia jinsi Daktari Mead angekuwa ameketi; jinsi ambavyo mtu mweusi angeingia, aketi hivi; na yote kulihusu.

⁸³ Ndipo asubuhi hiyo, nao wakasema...Mwanangu akaniambia, akasema, “Baba, ati utaenda kule kwenye ubishi huo?”

⁸⁴ Nami nikasema, “Siendi kule kubishana. Ninaenda huko, huku nimetiwa mafuta na Roho Mtakatifu, pamoja na Neno la Mungu litakalokilinda kiti kile cha rehema, almuradi Yeye yuko pale.”

⁸⁵ Kwa hiyo tulipofika huko chini, kabla hata hawajapata nafasi ya kuuliza jambo moja, Roho Mtakatifu akasema nami, kasema, “Sasa ndio wakati wa kulisema.”

⁸⁶ Nikasema, “Ninajua ni kwa nini mpo hapa.” Kisha nikasema, “Sasa, Ndugu Hicks, na wewe na Ndugu Carlson, kiongozi wa Wafanyabiashara Wakristo,” Nikasema, “hivi kila kitu hakiko vile hasa Roho Mtakatifu alivyoniambia juzi? Kwamba hamkukipata chumba hicho, tungekuwa hapa?” Nao ndio kwanza wakipate asubuhi hiyo. Nami nikasema, “Sasa angalieni, kila mtu amewekwa vile hasa Yeye alivyosema itakuwa.” Nikasema, “Jambo mnalotaka kunijia nalo ni juu ya Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ubatizo.”

⁸⁷ Basi wakati sisi... Roho Mtakatifu akaanza kulichukua Neno la Mungu na kulifunua na kulifasiri kabisa namna hiyo, wakati kundi hilo lote la wahudumu wa utatu limeketi pale, wakiinyosha mikono chini ya meza na kupeana mikono mmoja kwa mwingine huku machozi yakitiririka chini ya mashavu yao. Nami nasikia kwamba sabini na wawili kati yao wanashuka kuja kwenye maskani hii nipate kuwabatiza katika Jina la Yesu Kristo.

⁸⁸ Kiti cha rehema kimelindwa, mnaona, Roho Mtakatifu akikilinda kiti cha rehema. Hatuna budi kuliweka vivyo hivyo hasa... Acheni hilo Neno la Mungu... hao wajumbe mashuhuri wanaoketi pale, Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, ambao wanaunga mkono kila tendo la Agano hilo Jipya.

⁸⁹ Na sasa, sasa, hivyo ndivyo hasa vile nilivyosema kwenye sehemu ya kwanza ya ujumbe wa asubuhi ya leo, hebu na tukiweke papo hapo kimelindwa na Injili. Mnaona? Mnaona? Tukiweke papo hapo ambapo zile Injili zitakilinda.

⁹⁰ Sasa, tunaona mle ndani, walikuwa wakikilinda kiti cha rehema cha Mungu katika Agano la Kale; na pale, Mathayo, Marko, Luka, Yohana, hao wote. Na hata Simba wa kabila la Yuda aliutoa uhai Wake apate kukilinda kiti hicho cha rehema, akakiacha kinyunyiziwe Damu Yake Mwenyewe. Na Yeye huyo hapo amesimama asubuhi ya leo, leo hii, yule Mshindi mkuu ambaye atashuka kutoka Mashariki siku moja nasi tutamwona.

⁹¹ Sasa, tugeuke upesi, maana ninajua kuna ibada ya ubatizo. Kitabu hiki chenye mihuri saba ni nini? Loo, ni jambo kuu jinsi gani! Hivi mliona jinsi ambavyo linasema hapa, “Kulikuwa na mihuri saba upande wa *nyuma* wa hicho Kitabu”? Ni kitu fulani... Loo, Mungu na atusaidie sasa na atupe ujasiri, na labda siku moja ninaweza kuwaelezea. Angalieni, hili halijaandikwa katika Neno, limetiwa muhuri nyuma ya Neno. Hicho Kitabu

kilitiwa muhuri kwa hii mihuri saba. Siri yote ya hicho Kitabu imetiwa muhuri katika mihuri hii saba. Huu ndio mmoja wa milango iliyo mikuu sana kwenye Kitabu chote cha Ufunuo. Angalieni:

Kisha nikaona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi kitabu kilichoandikwa ndani. . . kilichoandikwa ndani (Kimeandikwa ndani, hayo ndiyo tunayosoma asubuhi ya leo.) na . . . nyuma, kimetwiwa muhuri saba.

Nje ya Biblia, yale ambayo Biblia hata haisemi, yametiwa muhuri hapa ndani kwa mihuri saba: siri za Mungu.

⁹² Sasa, ni kitu gani? Sasa, angalieni. Muhuri unawakilisha bidhaa iliyomalizika, kitu ambacho tayari kimejaribiwa, kikathibitishwa, na kisha kikatiwa muhuri. Ambapo kuna . . . Tunayo arabuni ya wokovu wetu sasa kwa kutiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo arabuni ya wokovu wetu.

⁹³ Hebu turudi nyuma kidogo tu. Ni—ninalo Andiko lililoandikwa hapa chini, kadhaa, sininii . . . sitakuwa na wakati wa kuyafikia yote. Lakini hebu turudi nyuma kwenye Waefeso, kwa muda kidogo tu, na kusoma ninii . . . katika mlango wa kwanza wa Waefeso, ili kwamba mweze kupata maana kamili.

Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu walioko Efeso, . . .

⁹⁴ Basi, kumbukeni, Yohana aliwaandikia Waefeso barua hii, kwa Efeso na walio waaminifu katika Kristo, wale ambao Paulo alikuwa amewahubiria na kuwalea, akawalisha kwa Injili. Mnaona?

. . . Efeso, na kwao wanaomwamini Kristo . . .

⁹⁵ Hiyo ni wale walio tayari katika Kristo. Tunaingiaje ndani ya Kristo? “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja,” ambao ni Mwili wa Kristo.

Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na . . . Bwana Yesu Kristo.

Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani yake Kristo Yesu:

⁹⁶ Liwazieni sasa! Yeye ametubariki kwa neema yote ya mbinguni, baraka, tunapokusanyika pamoja katika Kristo Yesu (kama waaminio, Kanisa teule, lililoitwa litoke, lililowekwa kando). Yeye ametutia muhuri kwa Roho Wake Mtakatifu, na sasa anatufunulia mambo yote yaliyo katika siku za usoni kwa ajili yetu. Sasa tumefika kwenye ile mihuri saba.

Kama vile alivyotuchagua sisi katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia . . . katika pendo:

Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wana kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake Mwenyewe. . .

⁹⁷ Hili ni wazo zuri jinsi gani! Hebu tuendeleo kusoma kwa dakika moja tu. Ninataka kufikia hapa chini hasa sana kwenye kifungu cha 12, na cha 13, cha 14:

Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sisi tuliotangulia kumtumaini Yeye.

Ambaye nanyi pia mmemtumaini, mkiisha kulisikia neno la kweli, na habari njema ya wokovu wenu: ambaye. . . baada ya. . . kumwamini yeye, mmetiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu,

⁹⁸ “Mkiisha kuamini.” Loo, ndugu yangu Mbaptisti, ungewezaje kusema Hilo sivyo lilivyo? Ati mnasema mnampokea Roho Mtakatifu hapo mnapoamini? Lilisema, “Baada ya kuamini ndipo mkatiwa Muhuri na Roho Mtakatifu wa ahadi.” Angalieni:

Ndiye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.

⁹⁹ Sasa, tunaona basi ya kwamba muhuri unamaanisha kwamba “ni jambo lililomalizika kwa Mungu, tayari limetatuliwa.” Na kila mwaminio alitiwa muhuri pamoja na ahadi hii tangu mwanzo, kwa sababu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu sisi tulitangulia kuchaguliwa kwa kufanywa wana wenye mamlaka. Kabla ulimwengu haujapata kuanza! Loo, ni tumaini la jinsi gani. Hilo linatufanya kutulia imara na thabiti. Nanga ya nafsi ambayo haitupwi huku na huko, bali imetia nanga katika Kristo, tumaini lililo thabiti. “Alituchagua tangu asili kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kufanywa wana wenye mamlaka kwa Yesu Kristo.” Loo, ni ajabu jinsi gani! Ninapenda hilo: “kazi iliyomalizika” kwa Mungu.

¹⁰⁰ Sasa, hebu niwanukulie tu Andiko lingine. “Wote aliowajua tangu asili, amewaita; wote aliowaita, aliwahasabia haki; wote aliwahasabia haki, amewatukuza.” Kote kote tangu mwanzo, Mungu, katika nia yake kuu isiyo na kikomo, alilionga Kanisa Lake tangu asili na kulichagua tangu asili lipate kufanywa wana wenye mamlaka kwa njia ya Yesu Kristo, apate kuwapa Uzima wa Milele mwishoni mwa wakati. Ni jambo zuri jinsi gani! Ndugu Neville, hilo linanifanya tu kujisikia vema zaidi. Na wewe je? Loo, naam. Kufanywa wana wenye mamlaka kwa Damu ya Yesu Kristo!

¹⁰¹ Sasa, angalieni tunapoendelea. Sasa, tunajua ninii iliyokwish-. . . Tumechaguliwa tangu asili pamoja na Mwana-kondoo. Roho Mtakatifu ndiye Muhuri wetu. Arabuni inamaanisha “kuna mengi zaidi yajayo.” Tuna arabuni Yake tu sasa. Arabuni ni malipo tu ya kwanza (Loo, ni nzuri jinsi gani!), ni malipo tu ya kwanza yanayoshikilia na kuyaweka salama

na kuyatia nanga kusudi mtu mwingine yeyote asiyaguse. Ni arabuni ya kufanywa kwetu wana wenye mamlaka. Amina. Roho Mtakatifu sasa ni arabuni ya Mungu mioyoni mwetu (kutiwa muhuri), kufanywa wana wenye mamlaka kunatungojea mwishoni mwa safari. Wana na binti za Mungu!

¹⁰² Hebu tugeukie Maandiko mengine, upesi sana, niliyoyaandika kwenye ukurasa huu mwingine hapa. Warumi 8:22, nafikiri ni zuri sana. Sasa, katika kusoma jana, kidogo niliandika Maandiko machache hapa ambayo ningetaka kuyarejea.

. . . tunajua ya kuwa—tunajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa.

Wala si hivyo tu, ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi yetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa miili yetu.

¹⁰³ Loo, mnaona jambo hilo? “Viumbe vyote vinaugua,” kasema Paulo. Kila kitu kinaugua. Angalieni miti jinsi inavyopambana. Angalieni maua jinsi yanavyopambana kwa ajili ya uhai; kisha tu jalidi kuyaangamiza. Angalieni miti jinsi inavyopambana kuyashikilia matawi yake yapate kuimba utukufu kwa Mungu. Mnaona? Kila kitu, viumbe vyote, wanyama wote, ndege wote, jinsi anavyoruka kumtoroka adui upesi na kutoweka, kila kitu kinaugua. “Na sisi pia,” kasema Paulo, “tunaugua, pia, pamoja navyo, kwa kuwa tunaungojea ukombozi wa mwili wetu.”

¹⁰⁴ Lakini sasa! Sasa! Yalifanya miaka hiyo yote mpaka sasa! Sasa tunayo arabuni ya urithi wetu! Loo, jamani! Tuna kitu gani? Tunalo thibitisho ya kwamba Mungu yu hai. Tunalo thibitisho ya kwamba Mungu yuko pamoja nasi. Tunalo thibitisho ya kwamba Mungu hajatuacha, ya kwamba sisi ni Wake na Yeye ni wetu, kwa sababu sisi (katika miili yetu), sasa tunaye Roho Mtakatifu mwilini mwetu anayelia, “Aba, Baba.” Wala hakuna kitu kinachoweza kumwondoa huyo. Tumetiwa nanga katika Kristo.

¹⁰⁵ Sasa, miti haina huyo, viumbe havina, bali hata hivyo tungali tunaugua pamoja navyo kwa kuwa bado hatujapokea utimilifu wa kufanywa wana wenye mamlaka. Lakini tuna arabuni yake, kwamba tuliokotwa kutoka kwenye mambo ya ulimwengu na sasa tukawa wana na binti za Mungu. Tunapaswa kuwa watu wa aina gani? Loo, jamani, tunapoliwazia hilo! Liwazie!

¹⁰⁶ Sasa tunayo arabuni, roho yetu inaugua kwa ajili ya kufanywa wana wenye mamlaka kikamilifu, bali sasa tunayo arabuni yake. Kwa kuwa tunampokea Roho Mtakatifu, ni arabuni ya kufanywa kwetu kikamilifu wana wenye mamlaka ama wokovu mkamilifu. Loo, ni nzuri jinsi gani! Ninalipenda tu hilo. Vema.

¹⁰⁷ Tunangojea ukamilifu wa kufanywa wana wenye mamlaka. Hili litatukia lini? Kwenye ufufuo wa kwanza. Hapo ndipo miili yetu itakapobadilishwa kutoka kwenye viumbe hivi viovu tulivyo sisi nasi tutakuwa na mwili kama Wake Mwenyewe uliotukuzwa, “Kwa kuwa tutamwona Yeye kama alivyo, nasi tutakuwa kama Yeye.” Hapo atakapoonekana, sisi tutaonekana katika sura Yake. Tutakuwa na mwili kama Wake, mwili mtukufu uliotukuzwa, na majaribu yote na mapambano ya maisha yatatoweka yakawa ukungu unaochukuliwa na upepo yasiweko tena.

¹⁰⁸ Na maskani hizi za duniani tunazougua ndani yake sasa, tunaingojea ile arabuni—ile arabuni. . . kwa wokovu mkamilifu kuja katika utimilifu wake. Lakini sasa katika maskani hizi za udongo tuna Kitu fulani kinachotwambia ya kwamba tumefufuka umbali huu. Amina. Arabuni ni nini? Ni malipo madogo ya kwanza yanayoishikilia, Ndugu Dauch. Ni arabuni. Sasa, wakati mmoja tulipoyapenda mambo ya ulimwengu, wakati mmoja tulipotenda dhambi na kuendelea kufanya mambo ya ulimwengu, wala hatukumjali Mungu, tulitengana na Yeye, pasipo na Mungu, pasipo na Kristo, ulimwenguni; sasa, Mungu alimtuma Roho Wake Mtakatifu na kupitia huyo tumeinuliwa kutoka kwa mambo hayo. Sasa tunayo arabuni, ya kwamba tunajua tumepita kutoka mautini kuingia Uzamani. Amina!

¹⁰⁹ Hapa, wakati nilipokuwa nikijaribu kuonyesha hili jinsi *hii*. Hapa ndipo ambapo mwenye dhambi wa kawaida hukimbilia, hapa chini. Sasa, Mkristo hupanda juu kidogo kuliko hapa, yeye huinuka juu ya upuuzi huo wote. Hiyo ndiyo arabuni ya wokovu wake.

¹¹⁰ Sasa, mpate kujua wakati. . . vile maono yanavyokufanyia. Basi nisaie, Mungu akiwa ni hakimu wangu, sikusudii kuwa na lingine. Likitokea, sitamwambia mtu, mnaona, maana ninaona vile lifanyavyo. Watu hawako tayari kwa ajili ya huduma kama hiyo, kwa hiyo inakubidi tu kuachilia liende, unaona, urudi hapa nyuma. Lakini kama nikipata kuingia hudumani tena, nitakuwa mwinjilisti. Lakini angalieni hapa. Kwenye hili hapa, tukirudi hapa ndani, huku juu, unaingia kwenye sehemu hii ya Kimbinguni hapa juu. Unaishi moja kwa moja kwenye zile milki kule. Unaenda mbali kupita chochote ambacho mwanadamu anaweza kuwazia, kupita chochote cha vitu hivyo. Nayo inakuleta kwenye hayo maeneo huko.

¹¹¹ Lakini, unaona, sasa tunayo, kwa Roho Mtakatifu, arabuni ya urithi wetu kwa sababu tumeinuliwa juu kutoka kwenye mambo ya ulimwenguni; nasi tunaendesha pamoja na walimwengu, lakini tuko juu ya walimwengu! Ee Ndugu Neville, Mungu aturehemu na kulijalia Kanisa la Mungu aliyehai . . .

112 Wakati kamwe tutakapofikia mahali kuwazia ya kwamba kanisa, kanisa zuri, kwamba, “Tunajaribu kujilinganisha na mambo ya ulimwengu. Tunajaribu kupata timu bora ya mpira wa vikapu kuliko waliyo nayo. Hatuna budi kuwa na je—jengo bora zaidi. Hatuna budi kuwa na mchezo bora zaidi wa karata. Hatuna budi kuwa na *hili* na *lile*, ama *linginelo* lililo bora zaidi.” Mbona, tunawezaje kamwe kulinganisha Hilo na madoido na kumeremeta kwa ulimwengu? Sisi si . . . Injili si *kumeremeta*; ni *kumeka*. Kunayo tofauti kati ya kumeremeta na kumeka.

113 Mnaona, tunazunguka tu huku na huku, kama nilivyosema, tukichukua maiti mo—moja kutoka nyumba moja ya maiti hadi nyingine, tukibadilisha wafuasi na vitu kama hivyo. Vema, ina faida gani? Na sisi tunajaribu kulifanya limeremete, minara mizuri mikubwa, mahali pazuri pakubwa mno. “Hatuna budi kuwa na lililo bora zaidi kuliko Methodisti ama lililo bora zaidi kuliko Baptisti, nasi sote tunajaribu kushindana na Katoliki, nasi tuna michezo ya karata na karamu na vyakula vya jioni na burudani, na kila kitu.”

114 Kanisa kamwe haliwezi kulinganishwa na ulimwengu. Unawezaje wewe pamoja na burudani za kanisa lako kujilinganisha na Shirika la Masoni ama—ama yeyote wa watu hao wanaoweza kufanya burudani? Hayo ni maeneo yao. Usijaribu kwenda kwenye maeneo yao.

115 Bali tunacho kitu Fulani wasicho nacho! Tunaye Yesu. Acheni waje huku kama wakitaka kitu. Dumuni katika Kristo. Tunaye Yesu. Wao hawataninii . . . hawawezi kuwa na Yesu mpaka waje huku. Ndipo tunapokuja huku, tumeondoka kwenye maeneo Yake.

116 Usijaribu kumetameta. Meka! Wala huwezi kumeka, unapaswa kumwacha Huyu ameke kupitia kwako. Unaona?

117 Maskini kimulimuli kidogo, yeye hameki kwa sababu anapenda kumeka; kwa kuwa yeye *kweli* humeka, kuna kitu ndani yake kinachomeka. Kiko ndani yake, ni yeye mwenyewe anayefanya hivyo, kitu fulani ndani yake kikimeka tu kupitia kwake.

118 Vema, hivyo ndivyo ilivyo na Roho Mtakatifu. Haitubidi tuwe wa kipekee, kuwa tofauti, kuwa kitu chochote zaidi, achilia tu na uishi maisha ya kitauwa na umwache tu Mungu aishi kupitia kwako. Hilo litameka kwa ajili ya Injili. Mnaona? Sio *kumetameta*; huko kunawafanya tumbili wavirukie vitu vya namna hiyo, chochote kinachometameta. Mnajua, hao sikuzote wanarukia kitu “king’aacho.” Bali *kumeka* ni “wororo, ulaini na utamu wa—wa Roho Mtakatifu.”

119 Sasa tunaungojea huo ufufuo. Vema, sasa, mnaelewa? Semeni “amina” kama mnaelewa, ninayomaanisha kwa kusema “arabuni.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Tumekuwa . . . Tu—tunajua tumepita kutoka mautini kuingia

Uzimani kwa sababu tumeinuliwa. Tumeinuliwa sio ndani yetu wenyewe, bali tumeinuliwa kutoka kwa mambo ya ulimwengu, hata tunampenda kila mtu. Naye Mungu anatupenda, nasi tunajua hilo. Nasi tunayaangalia maisha yetu na kuona ya kwamba ni Roho Mtakatifu, kwa sababu hatuyajali tena mambo ya ulimwengu. Mnaona? Haya basi. Mradi tu unaupenda ulimwengu au mambo ya ulimwengu, basi kumpenda Mungu hakumo ndani yako bado. Mnaona? Lakini mradi uko juu ya hayo, basi unajua ya kwamba unao urithi wako, unaona, uko—uko safarini kuelekea kwenye ukombozi wako mkamilifu.

¹²⁰ Pia, sasa, huo hautakuja, unaona, mpaka sisi kwanza... Kwanza hatuna budi kumwona Yesu. Ndipo atakapokuja, basi tutakuwa na mwili kama mwili Wake nasi tutafanywa kama Yeye. Vema.

¹²¹ Sasa, tunaona kitu ambacho kilipotezwa hapa (kwa sababu Biblia ilisema hivyo, na kwenye hiki Kitabu hapa) ambacho—ambacho kimetukombo. Tumekombolewa kutoka kwa nini? Kitu ambacho hapana shaka tulipoteza. Kabla hujaweza kukombolewa, lazima pawe na kitu kilichotukombo. Nao urithi wote tuliokuwa nao ume—umekombolewa. Basi hapana shaka tulikuwa na kitu fulani wakati mmoja tusicho nacho sasa, lakini Mwana-kondoo huyu anakuja kukombo. Mnaona? Tulikuwa na kitu tulichopotea kutoka kwake.

¹²² Sasa angalieni. Tulipoteza nini? Vema, Adamu alipewa kuwa na Uzima wa Milele, mradi tu alikula kutoka kwenye ule Mti alikuwa na Uzima wa Milele. Nasi tunaona tena kwamba Adamu alikuwa...yeye—yeye aliirithi dunia. Alikuwa ni... kama mungu mdogo juu ya dunia. Dunia ilikuwa ni mali yake. Kila kitu kiliwekwa mkononi mwake, angeweza kukitumia vyovyote alivyotaka. Alikipatia jina, akakiita, na kufanya lolote alilotaka. Yeye kweli alikuwa ni mwana wa Mungu.

¹²³ Sasa, katika kule kuanguka, Adamu aliipoteza hatimiliki yake. Aliiachilia kwa Shetani. Shetani akaichukua hiyo hatimiliki. Adamu alikuwa mzembe sana, wala hakuzikomboa haki zake kwa kuwa asingeweza kuzikomboa haki zake. Lakini Shetani, ambaye haimiliki kwa haki, bali anayo, yeye ndiye mungu wa dunia hii. Biblia ilisema hivyo. Anaimiliki hiyo. Si kwa sababu kwamba yeye—kwamba yeye—kweli anaipata kihalali, bali anayo. Sasa mnapata hilo? Shetani anayo hiyo, ameishikilia mkononi mwake. Mauti yako mkononi mwake, dunia iko mkononi mwake, ulimwengu ni wake, kila taifa ni lake, yeye anautawala na kuuongoza ulimwengu wote na kila kitu kilicho ulimwenguni. Shetani anautawala!

¹²⁴ Lakini Mungu na ashukuriwe sisi si wa ulimwengu. Mnaona? Kwa hiyo haya—haya basi. Mnaona? Na sisi ni...Simaanishi Kanisa; yeye halitawali Kanisa. Anautawala tu ulimwengu. Yeye alisema walikuwa ni wake, naye ni mungu wa ulimwengu. Yesu

alisema alikuwa hivyo, na ndivyo alivyo. “Yeye ni mungu wa dunia hii, ameyapofusha macho ya watu,” mungu wa dunia hii. Yeye ni Mungu wa Mbinguni. Na sasa kihalali yeye haimiliki hii. Si mali yake.

¹²⁵ Bali amepoteza ninii... Adamu aliipoteza hatimiliki yake, kwa huu, kitu hiki chote tulicho nacho, Uzima wa Milele na kuirithi dunia. Yesu alisema, katika Mathayo 5, “Heri walio wapole kwa kuwa watairithi nchi.” Mnaona? Sasa, hatunayo sasa.

¹²⁶ Basi, angalia, haikuwa kwa Adamu wala wowote wa uzao wake. Uzao wa Adamu kabisa ulipoteza kila kitu, pia. Sio uzao wa Adamu. Haijalishi ni jinsi gani tunavyojaribu kuupamba ulimwengu huu, na jinsi tunavyojaribu kujenga makazi makubwa na kadhalika, ungali si mali ya uzao wa Adamu. La, bwana. Haukumwendea uzao wa Adamu, la, bwana, kwa maana Shetani aliuchukua wote kabisa. Kweli! Kwa kuwa Adamu aliupoteza.

¹²⁷ Sasa, loo, jamani! Naam, mambo mengi sana yangeweza kusemwa. Si—sitaki kabisa kuchukua wakati mwingi kupita kiasi sasa, kwa hiyo hatuna budi, kubatiza. Vema.

¹²⁸ Yeye anayo bali si yake kihalali, Shetani anayo. Wakati mwenyewe halisi—mwenyewe halisi—mwenyewe alipoipoteza, kunayo njia moja tu inavyoweza kukombolewa. Sasa, hiyo ni kwa jamaa wa karibu, ndiye pekee anayeweza kuikomboa kisheria. Sasa, hakika, huyu tunaye katika kuzaliwa kibikira kwa Yesu Kristo.

¹²⁹ Sasa, ninataka kusema jambo fulani hapa. Jambo la kwanza tunalotaka kulirejea, ni, kama tukirejea kwenye—kwenye Agano la Kale hapa, ninaamini nimeliandika hapa chini mahali fulani, Mambo ya Walawi 25. Katika Mambo ya Walawi 25:23 na 24, unaweza kupata sheria za ukombozi, ninyi ambao mnaandika. Kukomboa chochote wakati mtu... Wakati Mungu alipowapa Israeli ninii yao... alipoigawa nchi yao kupitia Yohana, kila kabila na kila jamaa alipewa ardhi ambapo watoto wake walirithi ma—mali yake.

¹³⁰ Sasa, kama mtu huyu alifilisika na kupoteza chochote kwa mtu mwingine, huyu... na njia pekee kingeweza kukombolewa ilikuwa ni kwa jamaa wa karibu. Lakini hatimaye hakina budi kurejeshwa. Mtu huyu anakishikilia kwa muda fulani tu wa wakati. Lazima kirudi kwa mwenyewe wa asili. Kweli! Hakina budi kumrudia mwenyewe wa asili. Ninii... kama walikuwa wametoka katika kabila la Yuda, kama ilikuwa... Kama alikuwa kule na hii iligawiwa baba yake, basi ilikuwa ni kwake, ama jamaa fulani wa karibu angeweza kuichukua. Lakini, sasa, hakuna mtu mwingine aliyekuwa na haki... Wangeweza kuishikilia, wangeweza kuishikilia hatimiliki yake.

Wangeweza kuishikilia hatimiliki mpaka deni ilipolipwa, bali wakati mtu aliye na haki alipokuja, mtu ambaye. . .

¹³¹ Tuseme, kwa mfano, kama nilikuwa na kipande cha mali nami nikakipoteza, nami nikakiuzia Ndugu Neville ambaye ni wa kabila lingine, la Yuda, ama labda nikakiuzia mgeni. Naye anakimiliki kihalali, ni mali yake, angeweza kuingia mle na kuilima na kupata mazao kutoka kwake, na kadhalika, bali kwa kweli alishikilia tu ile hatimiliki. “Asingeweza kuimiliki,” hiyo ilikuwa ni sheria katika Israeli. Sasa soma katika—soma katika Mambo ya Walawi 25, nawe utaona ya kwamba wasingeweza kuimiliki kihalali; *aliishikilia* tu.

¹³² Vema, sasa, kwa mfano, mwanangu alitaka. . . Billy, huko nyuma, alitaka kuchukua ninii yangu. . . kuja kuinunua ardhi hii. Vema, basi, kama mgeni ama Ndugu Neville ama—ama mtu mwingine aliimiliki, alikuwa ameishikilia hatimiliki yake. . . Sasa, kama huyu alikuwa ndiye jamaa yangu wa karibu, alikuwa ni ukoo wangu, asingeweza kuishikilia tena. La, bwana. Ilimbidi kuiachilia, naam, bwana, hapo gharama hiyo ilipolipwa, wakati alipompa, tuseme, dola ishirini na tano elfu kwa hicho kipande cha mali.

¹³³ Vema, basi, tuseme, Ndugu Tony angekuja huku na kusema, “Ndugu Neville, nitanunua mali ya Ndugu Branham.” Asingeweza kufanya hivyo.

Ndugu Neville aseme, “La, bwana, sitaki kuiuza.”

“Vema, utatoa nini kwa ajili yake?”

“Ishirini na tano elfu.”

“Vema, ni—nitakupa elfu thelathini na tano. Nitakupa *hiki-na-hiki*.”

“Sijali unachotaka. Sitaki kuiuza, nitaiweka.”

¹³⁴ Lakini Billy Paul angeweza kuja na kusema, “Ninataka mali ya Baba yangu, hizi hapa elfu ishirini na tano zako.” Ilimbidi kuiachilia. Hiyo ni kweli, kwa sababu hiyo ilikuwa ni sheria.

¹³⁵ Loo, Haleluya! Humm! Natumaini ninyi Wakristo mnaliona. Sisi ndio chumvi ya dunia. Mungu aliwapa hii watoto Wake. Yeye alitupa utawala juu ya viumbe vyote, wanyama wote, uhai wote kila mahali. Lakini Adamu, baba yetu, akaipoteza kwa Shetani. Lakini inarejea wapi? Kwa Mwenyewe halali, Mungu Yule aliyeiumba. Amina!

¹³⁶ Si ajabu Yohana alisema “alilia sana,” kwa kuwa asingeweza kupata mtu aliyestahili kuikomboa. Huyu mtu hana budi kuwa anayestahili. Yohana alisema, “Nililia sana wakati hapakuwapo na mtu aliyeweza kukitwaa hicho Kitabu wala kukiangalia wala kuifungua mihuri yake.” Alisema, “Sio. . . Hakuna mtu Mbinguni, hakuna mtu nchini, hakuna mtu chini ya ardhi, hakuna mtu kila mahali.”

137 “Hakuna mtu.” Sasa, yeye kamwe hakuwapuuza Malaika. Kumbukeni, dunia hii haikupewa Malaika. Ni urithi wa mwanadamu. Gabrieli alistahili, hakika; mtu mwingine alistahili, huenda Mikaeli alistahili. Sio kama... Huenda alistahili kufanya hivyo. Lakini hakukuwako na mtu aliyestahili. Mnaona? Ndipo Yohana akalia kwa sauti kuu.

138 Mtu fulani alisema, “Kwa sababu alijikuta hastahili.” Sivyo ilivyo. Huyu mtu alikuwa chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, asingeweza kufanya kosa kama hilo. Ila a—alikuwa... a—alikuwa—alikuwa... Si kwamba tu hakustahili, asingeweza kumpata mtu yeyote aliyestahili.

139 Kwa hiyo mara hiyo tu akasema, “Mzee akaja ama malaika mwenye nguvu, kasema, ‘Usilie, kwa maana Simba wa kabila la Yuda,’” (Amina!) “‘Shina la Daudi, Yeye ameshinda!’” Amina! “‘Ameshinda,’ kwa maneno mengine. “‘Yeye anastahili kukichukua kile Kitabu!’” Amina.

140 Kumbukeni, hakuwa amemwona kufikia wakati huu. Kwa nini? Yeye alikuwa ameketi kwenye... ameketi kwenye Kiti cha Enzi mle ndani, Kiti cha Enzi cha Mungu. Alikuwa ndani ya yale madhabahu. Hakuwa amemwona hadi wakati huu, kwa hiyo Yohana alikuwa akitarajia kumwona Si—Simba akitokea, bali akamwona Mwana-kondoo!

141 Haya basi, ndugu. Kwa upole, kwa utamu, kwa Roho Mtakatifu tunashinda. Sio jitu kubwa mno la kiakili lenye nguvu, bali yeye anayeweza kujinyenyekeza ndiye mtu ashindaye. Mtu anayeweza kupigwa teke huku na huku na angali ni mtumishi wa Kristo, huyo ndiye mshindi.

142 Sasa, yeye alisema, “Yeye ameshinda. Na Yeye anastahili kukichukua kile Kitabu na kukifungua na kuifungua mihuri yake.”

143 Sasa, tutaona baada ya kitambo kidogo, labda sio leo, bali yale mihuri hii saba inayoshikilia, yale iliyofanya.

144 Sasa, hebu tuchukue kidogo juu ya “ukombozi.” Kabla—kabla mtu huyu hajaweza... hajaweza kukomboa, jambo la kwanza, ilimbidi kuwa anayestahili, ilibidi awe mtu anayefaa. Kwa hiyo hili lilitimizwa wakati Yesu Kristo alipozaliwa, kuzaliwa kibikira, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu. Alikuwa ni Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwanadamu, alikuwa Mungu katika mwili wa mwanadamu. Ilibidi awe anayestahili; nayo Damu ya kibikira ya Yesu Kristo ilimfanya kustahili. Sasa, tunaona ya kwamba, kama ukitaka kuyaendea Maandiko yake, ya Petro wa Kwanza 1:18 hadi 20 kama unayaandika hayo Maandiko chini. Ilibidi awe anastahili. Na Yeye alikuwa hivyo, kwa sababu alijitwalia mfano wa mwanadamu. Alifanyika mwanadamu, Mungu akawa wa jamaa yetu wa karibu. Na hapo tunaona basi ile sehemu nzuri ya Mungu Yehova aliyefanyika mwili akaishi miongoni mwetu kama Yule anayestahili. Amina.

145 “Yeye alishinda.” Mungu alichukua mfano wa mwili wa mwanadamu, akaja duniani, akazaliwa mtoto mchanga na kutembea miongoni mwetu. Na kupitia kwa Damu Yake takatifu Yeye akashinda.

146 Sasa, katika Agano la Kale, jinsi mwanadamu alivyopaswa kutangaza yake mwenyewe, yeye alifanya nini? Alimchukua mzee, wazee kumi, nao wakaenda langoni na kutambulisha yale aliyokuwa akifanya, kukomboa yale aliyokuwa amepoteza, na kuonyesha kwamba alikuwa ni nani, naye alitoa shahidi. Tunaiona hii hadithi ya kupendeza hapa (Kwa kuwa nilikuwa na muhtasari mdogo ulioandikwa hapa kuninii. . . nisije nikasahau, nikiwa na wasiwasi asubuhi ya leo.) juu ya Ruthu, jamaa wa karibu na Boazi. Tulipitia hilo sio muda mrefu uliopita. Ninawatakeni muone zile hatua tatu sasa za kupumzika huku.

147 Ninawatakeni muone kule kupumzika kwa Kanisa, jambo lile lile hasa. Sasa, tazama. Mahali pa kwanza tunaona, kwa kuwa sote tumepitia mahubiri hayo, *Mkombozi Wa Jamaa Wa Karibu*, Mungu alifanyika mwili apate kuwa Mkombozi. Alikuwa Ndiye hapa katika mlango wa 5—katika mlango wa 5. Kasema:

Wala hapakuwa na mtu mbinguni, wala juu ya nchi, wala chini ya nchi, aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama.

Nami nikalia sana, kwa kuwa hapakuonekana mtu astahiliye kukifungua hicho Kitabu ama kukisoma—ama kukisoma hicho kitabu, wala kukitazama.

Na mojawapo wa wale wazee akaniambia, Usilie: tazama, Simba aliye wa Kabila la Yuda, Shina la Daudi, yeye amestahili apate kukifungua kile kitabu, na zile muhuri zake.

Yeye Ndiye, Yeye ndiye Yule tunayemtazamia.

148 Angalieni jinsi Ruthu. . . jinsi. . . na Naomi, Boazi ni picha kamilifu tu. Jinsi ambavyo Naomi katika wakati wa njaa aliondoka kanisani, akaondoka nchini, akaenda kwenye nchi ya Moabu kukaa kule na kuwa mgeni mle ndani. Akapoteza yote aliyokuwa nayo. Ndipo wakati alipoondoka, mumewe, Elimeleki, akafa walipokuwa kule, kwa hiyo hiyo iliacha urithi wake umwangukie mtu yeyote. Ndipo tunapokuja. . . wakati anaporudi, anakuja pamoja na yule msichana mrembo mjane wa Moabu. Ndipo wakati Boazi alipomwona huyu mjane, mfano wa Kristo, alimpenda. Naye akampenda. Kwa hiyo, ilimbidi kukomboa, njia pekee aliyoweza kumpata awe mke wake ilikuwa ni kukomboa yale ndugu yake, Elimeleki, alikuwa amepoteza.

149 Na kwa hiyo basi akamwomba huyo ndugu yake mwingine kama angeikomboa, yule aliyekuwa wa karibu kuliko yeye, wala asingeweza kufanya hivyo. Kwa hiyo akashuka akafanye

mfano mkamilifu wa sheria za Mungu. Akaenda malangoni na kukivua kiatu chake, na kusema, “Na ijulikane leo hii ya kwamba nimekomboa yote aliyokuwa nayo Naomi. Yote aliyo nayo, yote ambayo Elimeleki (ndugu yangu) alipoteza, mimi ndimi jamaa wa karibu sasa, nami ndimi ninayeweza kuikomboa kwa hiyo nimekuja kuidai. Kama kuna mtu yeyote hapa anayeweza kuonyesha sababu ya haki ni kwa nini, ama mtu yeyote aliye wa karibu zaidi kuliko mimi, na ijulikane.” Na kila mtu akafunga kinywa chao. Kwa hiyo akakivua kiatu chake na kukitupa kwa ajili ya ushuhuda, “Nimekomboa yote ambayo ndugu yetu, Elimeleki, alikuwa nayo.” Kwa nini? Yeye alikuwa ni jamaa wa karibu. Alikuwa mkombozi wa jamaa wa karibu. Loo, ni la kupendeza jinsi gani! Ni hadithi nzuri sana.

¹⁵⁰ Ndipo basi, wakati huu wote, Ruthu alikuwa akipumzika na kungojea aone jinsi yangetokea. Kisha anarudi, hakuna mtu angaliweza kutoa ushuhuda dhidi yake. Alirudi na kumchukua Naomi... na kumchukua Ruthu, yule msichana mrembo Mmoabu, nao wakaoana na kuishi kwenye mali hii. Ni hadithi ya kupendeza jinsi gani!

¹⁵¹ Kunazo hatua tatu za Ruthu. Ruthu—Ruthu, *akiamua*; alikuwa akikata kauli kama angetoa uamuzi ama la, kurudi kwenye nchi ya uenyeji wake (kama tu vile Kanisa). Ruthu, *akitumika*; wakati alipoenda huko nje kuokota masazo. Ruthu, *akipumzika*; hiyo ndiyo Ruthu anayofanya sasa (Kanisa). Sasa Ruthu, *akizawadiwa*; sasa hapo ndipo, ama, jambo lingine linalotukia (ni zawadi ya Kanisa).

¹⁵² Sasa, hatuwezi... sina wakati, kwa sababu mna ibada ya ubatizo na ni saa tano kasorobo sasa. Lakini labda tutalichukua hili Jumapili ijayo ama Jumapili nyingine siku zijazo, Bwana akipenda. Nami ningependa kulichukua hili hapa, kuonyesha hizi pembe saba na macho saba, na hasa ile mihuri saba, zile huduma saba, malaika saba wa kanisa, nyota saba, sa-... Loo, hizo ninii chache...

¹⁵³ Na papa hapa panakifunga kitu hicho chote pamoja. Naam, bwana. “Ilibidi astahili,” kwa hiyo Yesu anastahili. Katika kurudi Kwake tutafurahia kikamilifu utimilifu wote wa baraka za ukombozi. Wenye upole watairithi nchi. Wanaume na wanawake watarudi: wana na binti za Mungu. Ndipo kile kipindi kikamilifu cha ule Utawala wa Miaka Elfu kitaanza. Ni jambo la kupendeza vipi!

¹⁵⁴ Naye Malaika mwenye nguvu kwa sauti kuu, akitangaza, “Ni nani anayestahili? Ni nani anayeweza kufanya hili?”

¹⁵⁵ Ndipo yule mzee akasema, “Usilie, kwa kuwa Simba wa kabila la Yuda, Yeye anastahili Naye ameshinda.”

¹⁵⁶ “Ndipo Yeye akakitwaa kile Kitabu na kukifungua Kitabu na kuifungua mihuri yake.” Hakusema kile kilichoipata. Tutakapofikia kufunguliwa kwa hiyo mihuri saba moja kwa

moja kote katika Biblia, angalieni kilichotukia. Moja kwa moja katika Kitabu hiki kilichotiwa mihuri saba tunachoingilia sasa, kinachoshikilia siri yote ya baraka zote za ukombozi wa Mungu. Kumbukeni, Yeye ni Mwana-kondoo, Yeye ndiye pekee aliyekomboa. Pia, kumbukeni, kimetiwa muhuri upande wa nyuma wa hicho Kitabu, hakijaandikwa ndani. Kimetiwa muhuri upande wa nyuma, wala hakijaandikwa ndani. Naye ndiye wa pekee aliyeweza hata kukifungua hicho Kitabu ama kukifunua hicho Kitabu ama kuifunua ile mihuri, Yule pekee aliyeweza kufanya hivyo.

¹⁵⁷ Kwa hiyo hili ni jambo moja, huenda wakazozania hili hapa, kwamba ni kitu gani, bali Yeye Ndiye ambaye anakifasiri kiungu. Lakini upande wa nyuma hapa hakuna mtu anayeweza kulifanya. Ni mali Yake na Yeye pekee, na Yeye Ndiye anayeweza kuzifunua hizo siri saba. Basi angalieni jinsi kila chembe yake ilivyo kwenye ukombozi, jinsi Kanisa lilivyokombolewa na ni kitu gani kitakachokomboa.

¹⁵⁸ Loo, hebu tumpende tu kwa mioyo yetu yote, tufanye yote tuwezayo.

¹⁵⁹ Mwandishi fulani alikuwa akiandika hadithi. (Kabla tu sijafunga na kumrudishia Ndugu Neville ibada.) Mnaufurahia Ufunuo? Loo, ninaupenda tu. Tuna yapata vifungu vitatu vyake tu asubuhi ya leo, bali tutauchukua tena. Angalieni. Tunaninii tu. . .

¹⁶⁰ Mwandishi mmoja alikuwa akiandika kitabu juu ya msichana mdogo aliyekuwa akijaribu kumtafuta Mungu.

¹⁶¹ Na mara nyingi sana ambapo tunamsaka sana Mungu na kumtafuta Mungu, na kama Mungu alikuwa kila mahali tu nawe. . . Alikuwa ni ninii mkubwa mno. . . Vema, kama angalikuwa na kiti cha enzi kikubwa mno hapa juu mahali fulani, kila Mtu angemwamini Mungu basi. Kama Mungu akiketi kwenye kiti kikubwa cha enzi hapa mahali fulani; tuseme, “Yeye ameketi kwenye mji fulani huu Naye huyu hapa. Huyu ni Mungu nawe umwende. Anaweza tu” [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] “kukigeuza namna *hiyo*,” mbona, kila mtu angemwamini. Basi imani ingekuwa ni bure. Haingetubidi kuwa na imani yoyote hata kidogo basi, mnaona, ingekuwa hivyo tu. Hiyo itakuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu, bali sasa Yeye anaita na kujaribu kupata kujua hao ambao. . . Linaonekana la kisiri na jeusi, na, hujui jinsi ya kulifanya. Lakini kwa imani tunaliamini! Tunaamini. Hiyo ndiyo sababu hili liko. Unaelewa hilo, Ndugu Elmer? Mnaona? Hilo. . .

¹⁶² Sasa, kama Mungu akiketi kwenye kiti cha enzi. Na kusema, “Mbona, Huyu hapa. . . Yule pale. . . huyu hapa Mungu. Anaishi kule chini mahali fulani, tutaenda kule chini.” Na kusema, “Mpendwa Bwana, Mungu, waweza kulifanya?”

“Naam, nitafanya hivyo.” “Psst!” Nalo lingetimizwa, mnaona. “Vema, hakika, huyo ni Mungu. Mnaona? Jamani, tunaona hilo.” Kwa hiyo kusingekuwa na haja... imani ingebatilishwa. Imani haina faida unapokuwa unalo.

¹⁶³ Vipi kama kila mtu humu ulimwenguni alikuwa ni Mkristo? Vipi kama kila mtu alikuwa—alikuwa ni Mkristo aliyejazwa na Roho? Mbona, tusingehitaji imani tena, tusingehitaji imani hata kidogo. Na imani ndicho ki—kitu chenyewe tunachookolewa kwacho, ni imani. Na hiyo ndiyo sababu hapana budi pawe na wengine wasiokubaliana Nayo, kusudi tuweze kuitumikisha imani. Mnalipata jambo hilo sasa? Huna budi kuwa na upande huo mwingine. Unaona? Huna budi kuwa na mwanamke mbaya kumfanya aliye halisi kudhihirika. Unaona? Inabidi kuwe na uongo kuifanya kweli dhahiri na kuifanya inawiri vizuri. Kama kila kitu kilikuwa ni Kweli, ingekuwa ni ya kawaida sana, unaona. Unaona? Lakini, unaona, ni kitu kizuri sana, ni kitu halisi, wakati Kweli na imani na kadhalika. Sasa, haya basi.

¹⁶⁴ Sasa, hatuna budi kuwa na hizi kweli na uongo. Hivyo ndivyo iendavyo. Inakubidi kuwa na siku nzuri kukufanya ufurahie... ama siku mbaya kukufanya ufurahie iliyo nzuri. Huna budi kuwa na ugonjwa mdogo kukufanya ufurahie afya nzuri. Unaona? Nawe huna budi kuwa na mabonde yako kukufanya uvifurahie vilele vya milima. Na kwa hiyo basi baadhi ya siku hizi yote itakuwa ni vilele vya milima, yote itakuwa ni afya, yote itakuwa ni Mungu, yote itakuwa ni furaha, ninii tu... kutakuwako—kutakuwako na furaha isiyo na mwisho. Lakini hadi wakati huo, mnaona, hatuna budi kuwa na haya mazuri na mabaya.

¹⁶⁵ Sasa, kila mtu anayeelewa hilo aseme “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.]

¹⁶⁶ Msichana huyu alikuwa akisema ya kwamba alikuwa akijaribu kumtafuta Mungu kila mahali alipoenda. Angeenda kwenye kanisa hili na kanisa lile, na chochote zaidi, wala asingeweza kumwona Yeye. Basi wakati mmoja akaona akishuka kwenda barabarani, kulikuwa na maskini mzee mmoja, akienda zake barabarani, jamaa mdogo, naye alikuwa amelibeba kanisa zima kubwa la jimbo mgongoni mwake. Alikuwa akitembea barabarani. Naye akasema, “Loo, mtu mwema!” Akasema, “Jamani, hilo ni zuri sana kwako,” kasema, “bali u—u—umekibeba kitu hicho chote mgongoni mwako.” Akasema... “Kitakuponda.”

Akasema, “La, hakitaniponda,” kasema, “kwa kuwa mimi ndimi ule Mwamba liliojengewa.” Huyu Ndiye.

Na tuombe:

¹⁶⁷ Ee Mwamba wa Nyakati, nina furaha sana kuwa nikiendesha tu katika kanisa kuu la jimbo, nikijua ya kwamba tumetulia juu ya ule Mwamba. Loo, Yeye alisema, ule Mwamba, “Sio zaidi ya

karatasi.” Ndipo wakati huo Mwamba ulipoanza kujongea upesi pamoja nayo, zile kengele za kupendeza zikaanza kulia ndani. Ee Mwamba wa Nyakati, tufiche ndani ya rehema Zako. Tushushe barabarani na kwenye kijito cha uzima ili kwamba mioyo yetu itajaa furaha na kuimba sifa Zako kote barabarani.

¹⁶⁸ Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya huku kutembelewa asubuhi ya leo na Roho Mtakatifu katika Neno, wakati Huyo akiingia na kulifanya Neno halisi sana kwetu. Tusamehe kupungukiwa kwetu na yote tuliyoifanya ama kusema yaliyokuwa ni mabaya, tusamehe hayo. Tusaidie kuwa Wakristo bora, Baba Mungu. Tunaomba ya kwamba rehema Zako zitatulia juu yetu.

¹⁶⁹ Naomba, Bwana, yakiwa ni mapenzi Yako, ya kwamba tungeweza kurudi tena karibuni sana na—na kumalizia milango hii hapa na kuichukua mihuri hii saba. Tuna—tunautazamia wakati huo, Bwana, ambapo Wewe—Wewe utaninii—Wewe utatujalia kufanya hivyo. Basi, Baba, papa hapa kwenye kanisa letu dogo tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia, tupate kuyafahamu mambo haya makuu ya Mungu. Sio kwa sababu kwamba tunastahili, Bwana, bali mioyo yetu yenye njaa ina hamu sana yake. Tunaomba kwamba Wewe utalijalia hilo.

¹⁷⁰ Tunamwomba Ndugu yetu Neville, Bwana, mchungaji wetu mwaminifu aliyetumwa na Mungu. Tunamwomba kwamba Wewe utamsaidia na kumbariki, yeye na maskini mke wake mwema sana, mzuri, na watoto wake wachanga.

¹⁷¹ Tunawaomba wadhamini wote na mashemasi na kila mtu anayehudhuria kanisa hili. Sio tu kwa ajili yetu, bali kwa ajili ya wengine na wote wanaoliitia Jina Lako. Ninawaomba marakiki zangu kutoka kote nchini, walipewa taarifa ndogo tu na hawa hapa. Baba, ni—ninakushukuru tu kwa ajili ya jambo hili.

¹⁷² Ninaomba ya kwamba utaiharakisha siku ambapo Yesu atakuja nasi sote tutakusanyika pamoja ambako hakutakuwako na mchana wala usiku tena, hakuna wakati tena, yote itaingia katika umilele na ambako sote tunaweza kuwa pamoja milele. Tujalie, Bwana.

¹⁷³ Na kukiwako na baadhi yao hapa asubuhi ya leo, Bwana, wasiokujua Wewe kama Mwokozi wao, jalia wapende kufahamiana na Mwana-kondoo Huyu anayeshikilia kile Kitabu cha kisiri kilichotiwa muhuri saba Mkononi Mwake. Mungu, jalia tufahamiane na Yeye kusudi katika siku za usoni wakati tutakapoiona hiyo mihuri imevunjwa na kufunguliwa basi tunaweza kuona yale Mungu anayotuzungumzia. Tunaomba hayo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kupitia Jina la Mwana Wake, Yesu Kristo.

Na huku tumeinamisha vichwa vyetu:

¹⁷⁴ Kungekuwako na mtu angesema, “Nikumbuke, Ndugu Branham, unapomba, nami ningetaka kukumbukwa katika

maombi”? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Na Mungu akubariki, na wewe, na wewe. Naam. Mungu awe mwema kwako. Naam. Labda mikono dazani mbili, ama zaidi, imeinuliwa.

¹⁷⁵ Ee Bwana, unaiona mikono yao, unajua haja yao. Unajua yaliyo moyoni mwao, sijui mimi. Ninaomba kwamba Wewe utawafunulia, Bwana, wema Wako na rehema Zako. Wape msamaha kwa lolote lile. Iwapo ni maradhi, Bwana, iponye miili yao na kuwapa afya. Fanya hivyo Baba, wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwa juu ya mkutano, juu ya kusanyiko sasa. Mungu mkuu wa Mbinguni na awatie mafuta sana hata atambariki kila mtu aliye kwenye Uwepo wa Uungu, ili tuweze kuondoka kutoka hapa asubuhi ya leo, tukisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?” Tujalie, Bwana.

¹⁷⁶ Sasa, mimi ni mnyonge na mchovu, sauti yangu imepotea, na mimi—mimi naomba tu, Mungu, kwa ajili ya nguvu zangu mwenyewe. Hivi Wewe utanisaidia? Utanipa nguvu? Lifunge maskini jeraha hilo huko chini, Bwana. Utafanya hivyo tafadhali? Jalia Mafuta Matakatiifu ya Mungu yaingie mle ndani, na katika kila jeraha lingine lolote, Bwana, kila mahali kwa kila mtu. Tunataka kuishi, Bwana, kwa heshima Yako na kwa utukufu Wako. Tujalie. Na uwaponye wagonjwa wote na wanaoteseka. Na—na ukipatie utukufu Mwenyewe, Bwana, maana tunatambua haitachukua muda mrefu mpaka tutaninii . . . hatutakuwa na mikutano hii tena; itaisha, itakuwa ni ya wakati uliopita.

¹⁷⁷ Sasa, Baba, bariki, sasa, tunaomba sote pamoja kupitia Jina la Yesu Kristo.

¹⁷⁸ Halafu, Baba, pia tungeomba ya kwamba Wewe utawakumbuka wale watakaobatizwa asubuhi ya leo katika Jina la Bwana Yesu, kwamba Wewe utawapa ubatizo wa Roho Mtakatifu, utukufu mkuu na heshima. Tujalie, Baba. Tunayakabidhi yote Kwako sasa.

¹⁷⁹ Pia, Baba, pamoja na hayo yote, ninajitupa ndani. Usinisahau, Bwana, nisaidie tu sasa. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.



UFUNUO, MLANGO WA TANO SEHEMU YA I SWA61-0611

(Revelation, Chapter Five Part I)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 11 Juni, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org